# SIFA ZA WATIIFU NO.2

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

SIFA ZA WATIIFU NO.2

WAFUASI WAKWELI WA MITUME

.?Ni alama gani zinazoonesha ukweli wa wafuasi wa Mitume *

.?Kuna athari gani katika kuwakubali na kuwafuata Mitume *

Katika makala iliyopita tulielezea kuhusu wafuasi wa kweli wa Mitume ya Mwenyeezi Mungu (s.w) na sifa walizonazo watiifu hao. katika makala hii tutaendelea kuelezea sifa nyengine .walizonazo watu hao

.Kunufaika na rehema zake Mwenyeezi Mungu .2-2

Kumtii Mwenyeezi Mungu na Mitume yake, kunamsaidia na kumuokoa mwanaadamu na ujahili, na pindi mwanaadamu akimtii Mwenyeezi Mungu na Mitume yake hujiepusha na kufanya madhambi, na mwanaadamu huyo hunufaika na rehema zake Allah (s.w). kama inavyosema -:Qur-ani Takatifu

وَاَطِيعُواْ اللّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ[1]

.mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa

Hapa inabainishwa kuwa rehema ya Mwenyeezi Mungu haiwezi kupatikana ila kwa KUMTII* Mwenyeezi Mungu na Mtume wake, kwa kufuata amri zao kiasi cha uweza wako, na kuwacha .makatazo yao kabisa kabisa

Haipatikani Pepo kwa kuwa wewe ni Muislamu tu (Mwislamu jina), wala kuwa unafuata madhehebu fulani ya Kiislamu au tarika (njia) fulani, kwa kuwa mkubwa wa madhehebu hayo .au mkubwa wa tarika hiyo atakushufaia

.Mtume mwenyewe atawapa watu shifaa kwa idhini ya Mola wake tu, seuze wengineo

Shida na mashaka, yatamsibu Sharia husema, Aso thawabu.

Huwa mbali naye, na kumwegema Shufaa ya Tumwa, Lmahbubu.

Siyahi na zite, katika moto Salili Jahimu, mambo mazito

Na kwenda miteo, na kugoroma Sura uwakao, kwa mivukuto.

Dhiki za motoni, ukadharau Dhamirini mwako, usisahau.

Wadhurubiyeo, wote Ulama Dhurubu mithali, kama hiyau.

Dhili ya Arishi, haketi tini Dhalimu wa huku, ulimwenguni.

Nyumba ya adhabu, zisizokoma Dhulma humpa, kwenda motoni.

Wale ambao humtii Mwenyeezi Mungu na Mtume wake, hufutiwa madhambi yao waliyoyafanya, na wala hawapunguziwi malipo yao hata chembe kutokana na mambo ya kheri .waliyoyafanya

-:(Kama anavyosema Allah (s.w

قَالَتِ الاَعْرَابُ آمَنَّا قُل لَّمْ تُؤْمِنُوا وَلَكِن قُولُوا اَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ الإِيمَانُ فِى قُلُوبِكُمْ وَإِن تُطِيعُوا اللّهَ وَرَسُولَهُ لاَ يَلِتْكُم مِّنْ اَعْمَالِكُمْ شَيْئاً إِنَّ اللّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ[2]

Mabedui wamesema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani Imani haijaingia katika nyoyo zenu. Na mkimt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hatakupunguzieni chochote katika vitendo vyenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye .kurehemu

.(Kunufaika na muongozo (usaidizi) wake Allah (s.w .2-3

Mitume, na wafuasi wa kweli wa Mitume hiyo hunufaika na muongozo wake Allah (s.w), na Mwenyeezi Mungu huwapa msaada watu hao duniani na Akhera. Kama anavyosema Allah -:((s.w

إِنَّا لَنَنصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِى الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الاَشْهَادُ[3]

Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na .siku watapo simama Mashahidi

Wema wasikate tamaa, watapata nusra tu japo itakuwa vipi – na japo baada ya kufa kwao, ya* .haki wanayoyalingania yatakuwa tu

MWISHO

Surat Al-Imrani Aya ya 132 [1]

Surat Al-Hujurat Aya ya 14 [2]

Surat Al-Ghaafir Aya ya 51 [3]